

DAIL NEWS, MONDAY, JULY 30, 2018

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI



NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI YA TAIFA

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Taifa (National Water Board). Bodi hii ni Bodi ya ushauri ambayo inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 Kifungu Na. 20. Muda wa Bodi ni miaka mitatu.

MAJUKUMU YA BODI

Majukumu ya Bodi kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ni kumshauri Waziri mwenye dhamana ya maji katika masuala mtambuka yanayohusu usimamizi wa rasilimali za maji, mipango shirikishi ya maji (integrated water resources management plans), utatuzi wa migogoro ya maji yenye sura ya kitaifa na kimataifa, usimamizi wa rasilimali za maji tunazoshirikiana na nchi nyingine (transboundary water resources management) na masuala ya kuhamisha maji kutoka bonde moja wenda bonde jingine (Inter-basin water transfer).

IFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji wa nafasi hii anatakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu katika masuala ya sekta ya maji au sekta zinazohusiana na sekta hiyo. Aidha, awe na ujuzi mahsusi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na asiwe/asitoke kwenye taasisi ambayo ni mtumiaji mkuu wa maji (major water user).

Maombi yatumwe kwa :

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maji na Umwagiliaji,
Tawi la NBC, Mazengo,
Barabara ya Kuu,
S.L.P. 456,
40473, Dodoma.

Maombi yaambatishwe na wasifu wa mwombaji (CV) yenye wadhamini watatu na namba zao za simu. Andika "Mwenyekiti Bodi ya Maji ya Taifa" nyuma ya bahasha.

Wisho wa kupokea maombi ni Jumatano tarehe 15 Agosti, 2018 saa 9.30 alasiri

Imetolewa na:

Prof. Kitila Mkumbo
KATIBU MKUU
WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI



NAFASI ZA WENYEVITI WA BODI ZA MAJI ZA MABONDE

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji na Umwagiliaji anatangaza nafasi za Wenyeviti wa Bodi za Maji za Mabonde yaliyoorodheshwa hapa chini. Bodi hizi zinaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 1 ya mwaka 2009 Kifungu Na. 21. Muda wa Bodi ni miaka mitatu.

- Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini
- Rufiji
- Pangani
- Wami/Ruvu
- Ziwa Victoria
- Ziwa Nyasa
- Ziwa Rukwa na
- Bonde la Kati.

MAJUKUMU YA BODI

- Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji, miradi, bajeti r mikakati ya Bonde husika.
- Kutoa miongozo na viwango vya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kuchukulia maji.
- Kukagua, kutathmini na kutoa vibali vya ujenzi wa miundombinu ya kuchepushia maji.
- Kufuatilia ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za rasilimali za maji..
- Kutoa au kufuta vibali vya kuchukuwa au kutupa majitaka.
- Kufanya utafiti, uchunguzi na kusimamia utoaji wa vibali vya kutupa majitaka ili kuzuia uchafuzi wa vyani vya maji,
- Kuratibu ushirikishwaji wa sekta mbalimbali katika usimamizi wa rasilimali za maji.
- Kumshauri Mkurugenzi wa Rasilimali za maji juu ya usimamizi wa maji shirikishi,
- Kuteuwa wajumbe wa Kamati za Maji za Mabonde Madogo (Catchment and subcatchment water comm tees).
- Kumshauri Afisa wa maji wa Bonde husika katika ugawaji na kusimamia matumizi bora ya maji kwen Bonde.

SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji wa nafasi hii anatakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu katika masuala ya sekta ya maji au sekta zinazohusiana sekta hiyo. Aidha, awe na ujuzi mahsusi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na asiwe/asitoke kwen taasisi ambayo ni mtumiaji mkuu wa maji (major water user).

Maombi yatumwe kwa :

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maji na Umwagiliaji,
Tawi la NBC, Mazengo,
Barabara ya Kuu,
S.L.P. 456,
40473, Dodoma.

Maombi yaambatiwe na wasifu wa mwombaji (CV) yenye wadhamini watatu na namba zao za simu. Andika jina Bodi ya Maji ya Bonde husika nyuma ya bahasha.
Mwisho wa kupokea maombi ni Jumatano tarehe 15 Mwezi Agosti, 2018, saa 09.30 alasiri

Imetolewa na:
Prof. Kitila Mkumbo
KATIBU MKUU
WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI